TANGAZO LA SERIKALI NA. 523 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29 (1))*

AMRI YA KUTANGAZA MABADILIKO YA MPAKA WA MSITU WA HIFADHI KIPEMBAWE YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Mabadiliko ya Mpaka wa Msitu wa Hifadhi Kipembawe ya Mwaka 2024.

Tangazo

Ts. Na. 258 la 1941

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Tangazo la Msitu wa Hifadhi Kipembawe linafanyiwa mabadiliko na kusomeka na kuonekana kama lilivyochorwa katika Ramani iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA CHUNYA


MSITU WA HIFADHI WA KIPEMBAWE

*Makadirio ya eneo:* Hekta 3365.60 au Kilometa za Mraba 33.66

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Msitu wa Hifadhi Kipembawe linalopatikana Wilaya ya Chunya, Mkoa wa Mbeya kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2883 ya mwaka 2013 iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

**KIPEMBAWE FOREST RESERVE**
**CHUNYA DISTRICT**
**AREA 3365.60Ha OR 33.66SQ.KILOMETRES**




Dodoma,
24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*